KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 15, Issue 3

23rd Dhul Qa'dah 1432

21st Oct, 2011

YALIYOMO

ADHABU YA KABURI, SABABU ZAKE NA NAMNA YA KUJIKINGA

ADHABU YA KABURI 1 - 4

Na: Imaam Ibn al-Qayyim al-Jawziyy (رحمه الله)

Shukrani zote ni za Allah, Mola wa viumbe wa Walimwengu na viumbe vyote na namswalia na kumtakia Rehma, Muhammad (صلى الله عليه وسلم) Mtume wake na mjumbe wake na ahli zake na Maswahaba wake.

SABABU YA ADHABU YA KABURI

Imam ibn al-Qayyim (رحمه الله) aliandika katika kitabu chake cha (ar-Ruh) akatanguliza kusema – "Huenda mtu akauliza, 'Ni sababu gani zinazomsababisha mtu kuadhibiwa kaburini?' Majibu ni mawili, moja kwa upana na jengine kwa muhtasar.

La muhtasar ni wanaadhibiwa kwa ujinga wao kumuhusu Allah na maasi yao wanayoyatenda katika yale waliyokatazwa. Allah hataadhibu roho iliyomjua ikampenda ikashikamana na maamrisho yake na kujiepusha na makatazo yake wala hataadhibu kiwiwili kilichobeba roho hiyo. Adhabu ya kaburini na ya akhera ni dalili ya ghadhabu za Allah kwa mja wake. Yule atakayemkasirisha Allah katika maisha yake duniani na akafa haliyakuwa hajatubia Allah atamuadhibu kulingana na kiasi cha makosa yake kaburini. Baadhi wataadhibiwa muda mfupi na wengine muda mrefu.

Jibu kwa kina ni maalezo ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyoeleza akisema kuhusu watu wawili alowaona wakiadhibiwa wakiwa makaburini mwao. Mmoja wao alikua akizunguka na khabari za urongo ili kutetanisha watu. Na wa pili alikuwa hajisafishi wala hajitwahirishi baada ya kukojoa. Wa pili aliacha amri ya kujitwahirisha baada ya kwenda haja na wa kwanza alitumia ulimi wake vibaya kwa kutetanisha watu hata kama yale aliyoyasema yalikuwa ni ya kweli. Kwenye maneno haya kuna dalili yakuwa Yule anayesema urongo na kueneza khabari zisizo sahihi ili kueneza uadui baina ya watu ataadhibiwa adhabu kali na vilevile kuna dalili yakuwa Yule ambaye ataacha swala ataadhibiwa vikali kuliko Yule ambaye hajitwahirishi baada ya kukojoa kwani kule kujiweka nadhifu ni sababu zinazohitajika kutekelezwa kabla ya swala. Katika hadeeth nyengine, Mtume (صلي الله عليه وسلم) atueleza yakuwa mmoja wa wale waliokuwa wakiadhibiwa kaburini alikuwa ni mtu aliyekuwa akisengenya wenziwe.

Katika hadeeth nyingine Mtume (صلي الله عليه وسلم) atueleza kuhusu mtu aliyechapwa kiboko kimoja akiwa kaburini mwake akasababisha kaburi lake kuwaka moto, hii ni kwa sababu aliwahi kuswali swala wakati fulani bila ya kuwa na wudhu,vile vile alipita pahali akaona mtu myonge akidhulumiwa akaacha kumtetea hali yakuwa angaliweza kufanya hivyo (at-Twahawee).

Imam al-Bukhari (رحمه الله) ametaja katika kitabu chake hadeeth ya Samurah ibn Jundub (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) alieleza kuhusu adhabu za baadhi ya watu kama vile yule mtu aliyeadhibiwa alikuwa akisema urongo na urongo wake ukaenea miongoni mwa watu. Mwengine alikuwa akihifadhi Quran

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

THE QUR'AN & SUNNAH HAJJ / 'UMRAH AGENCY

1432HIJRI/ 2011 C.E

Assalaamu 'Alaykum Warahmatullaahi Wabarakaatuh:
Tunafuraha kuwajulisha yakwamba Insha Allaah mwaka huu 1432 Hijri/ 2011, tumeanza Barnaamij ya kupeleka watu Hajj.

Mipangilio Ya Safari

- Kuondoka ni katika wiki ya mwisho ya mwezi wa Dhul Qa'dah
- Kurudi ni mwisho wa mwezi wa Dhul-Hijjah
- Safari itaanza Mombasa – Nairobi – Jeddah
- Kurudi ni Jeddah – Nairobi – Mombasa
- Gharama ya Safari (ikiwemo Hoteli, Usafiri na Chakula – mara 3 kwa siku tukiwa Mina kwa siku tano)
- Class "B" ni $3800 U.S Dollars / Class "C" ni $3200 U.S Dollars
- Amma mas'ala ya Chakula (Makka na Madinah) kila mtu ni juu yake
- Tutakuwa na Darsa juu ya mas'ala ya Hajj kabla ya kuondoka na tutakapokuwa Makkah
- Tutaandamana na Daktari wetu kutoka hapa Mombasa Insha Allaah

Kwa Maelezo Zaidi

Fika katika Maktaba ya QSS iliyoko ubavuni mwa Tajj Hotel (Duka la tatu baada ya Duka la vitabu vya Dini), au
Wasiliana nasi kwa kutuandikia barua Pepe kwa info@qssea.net, au
Tupigie simu nambari mojawapo ya hizi zifuatazo:
+254 723471820 au +254 721473181, au +254 700365253

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

lakini alikuwa akilala usiku kucha wala haamki kuwsali tahajud na alikuwa hatekelezi mafunzo yake mchana. Mtu wa tatu ni kundi la watu lilokuwa likitenda maovu ya uzinifu na wengine walikuwa wakila mali yaliopatikana kwa njia ya riba na Mtume (صلي الله عليه وسلم) alieleza kuhusu watu hawa wote kwani aliweza kuonyeshwa wakiwa waadhibiwa katika makaburi yao.
Na kwenye hadeeth nyegine Mtume (صلي الله عليه وسلم) aeleze kuwa baadhi ya watu walikuwa vichwa vyao vikipasuliwa mapande mapande kwa mawe makubwa kwa sababu walikuwa wakilala ilhali hawajaswali na wakizipuuza bila ya kuziswali.Vile vile Mtume (صلي الله عليه وسلم) alitueleza wengine walilishwa mti wa az-Zaqqum (huu ni mti ulioko jahanam) kwa sababu walikuwa hawalipi zakaah. Wengine watakula nyama mbovu zilizo oza kwa sababu walikuwa wakizini na wengine midomo yao yamekatwa kwa sababu walikuwa wakileta mizozo baina ya watu katika nyakati za fitna.
Vilevile Mtume (صلي الله عليه وسلم) alitueleza kuhusu mtu aliyechukua nguo ya ngawira bila ya kumjulisha Mtume (صلي الله عليه وسلم), ikawa sababu ya ile nguo kubadilika moto na kumchoma kaburini mwake.
Adhabu ya kaburi ni matokeo ya madhambi yaliyofanywa kwa moyo, macho, masikio, vinywa, ulimi, tumbo, tupu, mikono, miguu na mwili mzima. Yafuatayo ni baadhi ya madhambi yenye kusababisha adhabu ya kaburi;

* Kueneza habari za urongo - kusengenya na kutukana.
* Kutoa ushahidi wa urongo.
* Kuleta utata baina ya watu.
* Kuzua kwenye dini.
* Kuzungumza kwa niaba ya Allah (سبحانه وتعالى) na Mtume (صلي الله عليه وسلم) bila ya 'ilmu.
* Kula riba na milango yote ya riba.
* Kula mali ya yatima bila ya haki.
* Kuhusika kwa njia moja au nyingine na rushwa au hongo.
* Kula mali ya Waislamu wenzio au mtu uliye na ahad naye bila ya haki.
* Kunywa venye kulewesha kama pombe na vyengine.
* Uzinifu na uliwati.
* Wizi na umwagaji damu na kuuwa bila ya haki.
* Udangayifu, kufanya khiyana na ulaghai.
* Kutumia urongo kubadili yale yalio halali ukayafanya haramu na kinyume chake kwenye Uislamu au kuzuia watu kutekeleza wajibu wao wa dini na kuhimiza watu kuyafanya yaliokatazwa na Allah.
* Kuudhi Waislamu na kuyawinda makosa yao.
* Kutoa hukmu bila ya kutumia hukmu ya Allah (سبحانه وتعالى) au kutoa hukmu zilizo tofauti na hukmu za Allaah.
* Kusaidia madhalimu na watu waovu.
* Kupotoa na kupindua maana ya majina na sifa zake Allah (سبحانه وتعالى) au kutoamini.
* Mtu kupa kipa-umbele maoni yake na mapenzi yake au siasa juu ya Sunnah ya Mtume (صلي الله عليه وسلم) au kutukana as-Salaf as-Swalih (watu wema waliotutangulia wa umma wa Ki-Islam)
* Kuwa ni mwanamke aliyeajiriwa na jamii yenye msiba kulia kwa kilio kikubwa na wale wanaokaa ili kumsikiza.
* Kuwa muuimbaji au msikizaji mziki.
* Kujenga misikiti juu ya makaburi.
* Kupunguza vipimo wakati upimiapo watu na kuongeza vipimo pindi upimiwapo wewe.
* Udhalimu, kiburi, maringo na kusaidia wenye sifa hizo.
* Kuwa jabari unapoamrishwa mambo ya Allah lakini ukawa na khofu unapotishwa na binadamu wa kawaida.
* Kusoma Quran na usiathirike nayo, na hata kushughulika na mambo mengine unapoisoma; lakini ukisikiza mziki, ambao ni utangulizi wa kwenye uzinifu na kiungo katika viungo vya unafiki, ukafurahi na ukawa mweye kushangilia na ukatamani mziki huo usikome.
* Kutoa ushahidi wa urongo na kuapa kwa jina la Allah na kusema kweli unapo apa kwa jina la sheikh, baba, kiongozi au yeyote umpendae.
* Kujivuna na kujigamba kwa madhambi yako.
* Kutokuwa muaminifu na mali au heshima za watu.
* Kuwa na ulimi mchafu, watu wakakuepuka kwa hofu ya uovu unaoweza kusababisha.
* Kuakhirisha swala mpaka wakati ukatoka, kisha ukaswali kwa haraka.
* Kulipa zakkat ilhali ya kuchukia ila unapolazimishwa.
* Kutohiji ingawa ulikuwa na uwezo wa hali na mali.
* Kutotekeleza haki za watu ijapo una uwezo wa kutekeleza jambo hilo.
* Kutomjali Allah katika mapato na rizki yako.
* Kukata kizazi.
* Kutokuwa na huruma na wenye kuhitaji (mafukara na masikini), wajane na mayatima.
* Kutokuwa na huruma na hayawani.

Mifano ya watu wote tuliowataja na wengine wenye mifano kama hiyo wataadhibiwa makaburini mwao kwa uhalifu wao. Kila mmoja atapata adhabu kwa kima cha uhalifu wake. Na wote wataadhabiwa isipokuwa aliyetubia, hakika Yeye, Allah ni mwingi wa Msamaha na Huruma.

VIPI KUJIEPUSHA NA JANGA LA ADHABU YA KABURI

Imam ibn al-Qayyim (رحمه الله) amesema: "Kwa ujumla, kujiepusha na yenye kusababisha adhabu kaburini ndio njia bora ya kuepuka adhabu ya kaburi. Mtu atakiwa akae kwa muda kabla hajenda kulala usiku na ajituhumu nafsi yake kwa aliyofaidika nayo siku hiyo na aliyokosea, kisha atubie upya kihakika mbele ya Mola wake kisha alale baada ya kutubia. Na pindi aamkapo awe na hima kubwa ya kutoregelea maovu na kujihimiza kutenda mema. Afanye hivyo kila usiku; akifa usiku ule atakuwa katika wale waliotubia na waliojiepusha na adhabu ya Allah (سبحانه وتعالى) na akiamka hai atakuwa ni mwenye furaha kwa kuwa atakuwa amepewa fursa nyingine ya kuongezea thawabu na amali njema kurekebisha yale aliyoyakosa. Hakuna namna nyingine iliyo bora kama kuangukia kitanda chako usiku kwa namna hii. Njia iliyo na faida katika maisha ya Muislamu, haswa ikiwa Muislamu atakuwa na mafungamano mazuri na amri za Allah katika kuandama hisabu hii kwa kumtaja Allah kama ilivyofundisha Sunnah katika namna ya kulala na kuomba dua mpaka akatwaliwa na usingizi. Yule Allah anayemtakia kheri, basi Allah atamuzesha kufanya hivyo.
Kwa ujumla tunakumbusha watu hadeeth za Mtume (صلي الله عليه وسلم) alizotueleza baadhi ya njia zinazomuokoa mja na adhabu ya kaburi.
◊Katika hadeeth iliyopokewa na Salman al-Farisi (رضي الله عنه) kutoka kwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) yakuwa amesema: "Ribaat (kulinda safu za jeshi la Waislamu) kwa siku moja ni bora thawabu zake kuliko kufunga saumu mwezi mzima na kuswali usiku wake; na yule atakaekufa akiwa katika hali hiyo atakuwa na malipo ya matendo ambayo aliyokuwa akiyafanya yakiendelea (malipo hayo) mpaka siku ya kufufuliwa na ataokoka

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

na adhabu ya kaburi " [Muslim].

* Mmoja wa Maswahaba wa Mtume (صلي الله عليه وسلم) allimuuliza Mtume (صلي الله عليه وسلم): "Ewe Mtume wa Allah, kwanini watu wote wapata mitihani makaburini mwao ila mashahidi?" Yeye Mtume (صلي الله عليه وسلم) akajibu: "Panga zipitazo juu ya vichwa vyao ni mtihani wa kutosha [An-Nasaa'i].

* al-Miqdaad ibn Ma'd Yakrib (رضي الله عنه) amepokea kutoka kwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) akisema: "Shahidi ana alama saba nzuri alizopewa na Allaah: atasamehewa kwa kutokwa na tone la kwanza la damu yake, ataona kiti chake au makao yake peponi, ataokoka na adhabu ya kaburi, ataokoka na kitisho kikubwa siku ya kufufuliwa, atavaa nguo maalum ya fahari ya imani ataoa wanawake 72 wa peponi na ataweza kuwashufaiya watu sabiini katika familia yake [at-Tirmidhee]. Kwenye hadeeth nyingine asema Mtume (صلي الله عليه وسلم): "Taji la heshima litavalishwa kwenye kichwa chake, kila taji la heshima litavishwa kichwani mwake, kila taji likiwa ni bora kuliko ulimwengu huu na vilivyomo ndani yake, atakuwa na wake sabiini na mbili katika wake wa Jannah na ataruhusiwa kuomba shifaa kwa watu sabiini kutoka katika jamii yake [At-Tirmithi].

* Abu Hurayrah (رضي الله عنه) alihadithia kutoka kwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) kuwa alisema: "Kuna sura ndani ya Quran [AL-MULK] yenye aya thalathini, itamshufaia yule mwenye kuisoma kwa kuendelea mpaka akapata msamaha." [An-Nasaa'ee na Ibnu Maajah]. Hadeeth hii na nyingine zenye maana sawa ni dalili yakuwa wale wanaoisoma surat al-Mulk kila mara na kutekeleza mafunzo yake wataokolewa na adhabu ya kaburi. Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema; "Atakaekufa kutokana na maradhi ya tumbo hatoadhibiwa kaburini mwake." [At-Tirmithi]. Malipo haya yatawafikia wale ambao watakuwa ni wenye kusubiri wakati wa Maradhi yao wala hawakati tamaa na Rehma ya Allah.

* Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: "Allah atamuhifadhi yoyote katika Waislamu na fitna ya adhabu ya kaburi akifa siku ya Ijumaa, iwe ni usiku au mchana." [Ahmad].

* Katika ukamilifu wa imani Allah (سبحانه وتعالى) amesema: **"Hakika wale wanaosema Mola wetu ni Allah Peke yake, kisha wakawa na misimamo ya kisawasawa [kwenye Tawheed na Sunnah], hakika juu yao hamna hofu wala hawatohuzunika."** [Al-Ahqaaf

KILIO CHA MTUME MUHAMMAD (صلى الله عليه وسلم)

Na: Sheikh Hussein al-Awaysha

Imepokewa kutoka kwa al-Baraa Ibn Aazib (رضي الله عنه) aliyesema: 'Siku moja tulipokuwa na Mtume (صلي الله عليه وسلم), kwa ghafula aliona kundi la watu, kisha akauliza: "Ni kitu gani kilichowakutanisha watu hawa hapa?" akajibiwa: "Wamekuja kuchimba kaburi." basi Mtume (صلي الله عليه وسلم) akashtuka na kuwa na khofu na kwa haraka akenda mbele ya Maswahaba zake mpaka akalifikia kaburi, kisha akapiga goti juu yake, na mimi nikamuelekea kumkabili uso wake (صلي الله عليه وسلم) ili nimuone afanyalo. Mtume (صلي الله عليه وسلم) akaanza kulia mpaka ardhi ikaroa kwa machozi yake, kisha akatugeukia sisi na akatwambia: *"Enyi Ndugu zangu! Jitayarisheni kwa siku kama hii."*

Imepokewa kutoka kwa Ali (رضي الله عنه) aliyesema: "Sisi hatukuwa na mpanda Farasi katika siku ya *Badr* isipokuwa *al-Miqdaad.* Sote tulikuwa tumelala isipokuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) aliyekuwa chini ya mti, akiswali na huku akilia mpaka kulipopambazuka."

NENO LA BUSARA

Amesema Mtume (صلي الله عليه وسلم):

"

Toobah ni kwa yoyote mwenye kuumiliki Ulimi wake, ambaye Nyumba yake inamtosheleza [(yaani; ametosheka nayo) na mwenye kulia kutokana na madhambi yake.

"

Toobah ni mti wa Peponi wenye ukubwa wa umbali wa miaka mia moja.

(Ahmad na wengineo, ni hasan lighayrihi, as-Swaheehah)

(Endelea kutoka Vol.15, Issue 2)

AL-MAHDI, MUHAMMAD BIN ABDULLAAH

Vilevile Ahmad, Abu Daawud, Ibn Maajah na Ibn Hibban wamepokea yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Nyinyi pamoja na ar-Rum mutaafikiana mkataba wa kuwavamia maadui kutoka nyuma yenu na mutasalimika, mujipatie mali ya nyara. Kisha mutaweka kambi yenu katika **Marj Dhi Tuloul**. Kisha Mrumi mmoja atasimama, auinue msalaba na aseme, **"Msalaba umeshinda kwenye vita!"** Atasimama Muislamu na amuuwe huyo Mrumi. Warumi watavunja mkataba, na al-Malahim itaanza. Wataandaa jeshi lao wapambane na nyinyi waje kwa makundi thamanini, na kila kundi likiwa na (majeshi) elfu kumi."*

Katika riwaya nyengine, Abu Maalik al-Ashja'ee amesema yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Patakuwa na mkataba baina yenu na wenye nywele za kizungu (ar-Rum) na watavunja mkataba wenyewe. Kisha watawajia nyinyi wakiwa makundi thamanini, na kwa kila kundi wakiwa (wanajeshi) elfu kumi na mbili.*

Wakati wa al-Malhamah, *fustat* (kambi ya kijeshi) ya Waislamu itakuwa ***al-Ghoutah***, sehemu iliyozunguka mji wa Damascus. Abu ad-Dardaa' amepokea yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Fustat ya Waislamu, wakati wa al-Malhamah itakuwa mji kwa jina la Damascus, miongoni mwa miji bora ya ash-Shaam."*

Katika riwaya nyengine, amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Fustat ya Waislamu, wakati wa al-Malhamah Kubwa itakuwa kwenye ardhi iitwayo al-Ghaoutah, katika mji uitwao Damascus, mahali bora pa Waislamu watakapokuwepo."*

Hapo ndipo mahali ambapo Waislamu kutoka ash-Shaam, bara Arabu na sehemu nyengine za Waislamu watakapoungana kupambana na maadui wa Allaah. Waislamu wote hawa, wakiwemo *mawali* wataungana juu ya Dini ya Allaah, wakipigana pamoja na ndugu zao kwa ajili ya Allaah.

Amepokea Ibn Maajah yakwamba Abu Hurairah amesema kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Vita vitakapoanza, Allaah ataleta mawali watakaokuwa na Farasi bora miongoni mwa Waarabu, na silaha bora. Allaah Ataipa Dini ushindi kwa kupitia wao."* Twamuomba Allaah auunganishe Ummah huu na auondolee *Ujahiliyyah* na *ikhtilafu* miongoni mwao.

(Endelea kutoka Uk. 3)

Allaah Atawapa ushindi Waislamu wakiwa al-Malhamah na wataishinda Constantinople bila ya kutumia silaha za kuingia humo. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Mushaisikiya Nchi iliyozungukwa na ardhi kwenye upande mmoja na kwa Bahari kwenye upande mwengine?"* Wakasema, "Na'am, Yaa Rasoolullaah." Akasema, *"Kiyama hakitokuja mpaka vizazi elfu sabiini vya Isma'eel wavamie hapo. Watakapofika hapo, wataweka kambi bila ya kuwa na haja ya kutumia silaha au kurusha mshale kwa ajili ya kupigana. Wao watasema, "Laa llaaha illallaah wallaahu Akbar." Kisha sehemu yake moja (Ukuta wa Mji) ulio pambizoni mwa Bahari utabomoka. Watasema kwa mara ya pili*, '*Laa llaaha illallaah wallaahu Akbar,' na upande wa pili (ukuta ulio pambizoni mwa ardhi) utabomoka. Watasema kwa mara ya tatu, 'Laa llaaha illallaah wallaahu Akbar', na kutakuwa na matundu makubwa (ndani ya kuta zake) yenye nafasi zenye kuwatoshea wao kuingia na wakusanye mali za nyara. Pindi watakapokuwa wakigawanya mali za nyara, atawajia mpiga mbiu, huku akisema, "ad-Dajjaal ashatokeza."* Kisha watawacha kila kitu na warudi (ash-Shaam)."

USHINDI WA WAISLAMU KABLA YA KUJA KWA AD-DAJJAAL

Jaabir bin Samurah amepokea, "Naafi' bin 'Utbah amesema, 'Tulikuwa pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwenye vita'. Kisha (Naafi') akasema, 'Kisha baadhi ya watu kutoka katika sehemu za Magharibi (ya Madinah) wakaja kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) wakiwa wamevaa nguo za Sufi wakakutana nae karibu na kilima. Walikuwa wamesimama haliyakuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) ameketi.' Kisha (Naafi') akasema, 'Basi nikajiambia nafsi yangu, "Hebu nijisongeze karibu yao nipate kusimama baina yao na yeye wasije wakamdhuru (au wakamuuwa)." Kisha (Naafi') akasema, '(Kisha nikajiambia nafsi yangu), "Huwenda wakawa na mazungumzo nae." Lakini hata hivyo, nikajikurubisha zaidi mpaka nikasimama baina yao na yeye.' Kisha (Naafi') akasema, 'Kisha nikahifadhi misemo minne kutoka kwake, na naweza kuihesabu kwa mkono wangu. Akasema: "Mutavamia Bara - Arabu na Allaah Atawapa (nyinyi). Kisha (mutaishinda) Fursi na Allaah atawapa (nyinyi). Kisha mutaivamia ar-Rum na Allaah atawapa (nyinyi). Kisha mutamvamia ad-Dajjaal na Allaah atawapa ushindi (nyinyi)." Kisha Naafi' akamwambia Jaabir, "Ewe Jaabir! Sisi hatuamini yakwamba ad-Dajjaal atajitokeza mpaka ar -Rum ishindwe."

Nchi ya ar-Rum ni Ulaya (Europe) na Rome ndio moyo wake. Mtume (صلى الله عليه وسلم) ametubashiriya sisi yakwamba tutaishinda Rome, makao makuu ya Ukristo leo, baada ya Waislamu kuyashinda Makao makuu ya kwanza ya Ukristo, Constantinople.

Imaam Ahmad amepokea yakwamba Abdullaah bin 'Amr bin al-'Aas amesema: "Tulipokuwa tumekaa na Mtume (صلى الله عليه وسلم), tukiandika hadeeth, Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliulizwa, "Ni nchi ipi katika mbili hizi itakayoshindwa mwanzo, Constantinople au Romiyah (Rome)?' Akasema, 'Mji wa Heraclius ndiwo utakaoshindwa mwanzo.' Alimaanisha Constantinople.'"

(Endelea kutoka Volume 15, Issue 1)

'ISSA (عليه السلام) MWANA WA MARYAM

Vilevile al-Bukhaari, Muslim, Ahmad, at-Tirmidhee na Ibn Maajah wamepokea yakwamba Abu Hurairah amehadeetha yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Naapa kwa Aliyeimiliki nafsi yangu! Wakati umekurubia kwa mwana wa Maryam awajilie nyinyi, atakuwa ni kiongozi muadilifu na Imaam mwenye msimamo wa kisawasawa. Atavunja misalaba, awauwe Nguruwe, ataamrisha AL-Jizyah itolewe, na pesa zitakuwa nyingi mno kiasi cha kwamba hakuna atakaekuwa na haja nazo. Kisha Sijdah moja itakuwa ni bora kuliko Uiimwengu mzima na kila kilichomo ndani yake.* Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema yakwamba 'Issa atafanya Hajj kwenye Nyumba Tukufu ya Makkah. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "*Naapa kwa Aliyeimiliki nafsi yangu! Kutoka Fajj ar-Rawhaa [mahali fulani karibu na Makkah], 'Issa mwana wa Maryam atatangaza yakwamba atafanya (atatekeleza) Hajj, Umrah au zote kwa pamoja."*

Pia Mtume (صلى الله عليه وسلم) ameyaeleza maisha katika wakati atakapokuja 'Issa mwana wa Maryam kwa mara ya pili akasema: *"Maisha ya baada ya 'Issa yatakuwa na Baraka nyingi. Mbingu zitaruhusiwa kupeleka mivua yake na ardhi zitatoa mazao yake kiasi cha kwamba hata ukimwaga mbegu zako juu ya majabali magumu, basi zitamea! Atapita mtu mbele ya Simba na hatodhuriwa nae na amkanyage nyoka na hatodhuriwa nae. Kisha hapatokuwa na uadui, wivu wala chuki."*

Mtume (صلى الله عليه وسلم) akatoa bishara njema kwa wale watakaopigana vita wakiwa pamoja na 'Issa. Kikosi hichi ndicho kilichobaki cha *at-Twaaifatul-Mansoorah* ambacho kitakachokuwa daima ni chenye kuinua bendera ya Uislamu iliyoinuliwa mwanzo na Mtume (صلى الله عليه وسلم) na Maswahaba zake. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Allaah Ametoa kinga kutokamana na Moto kwa makundi mawili miongoni mwa Ummah wangu: Kundi litakalovamia India na kundi litakalokuwa na 'Issa, mwana wa Maryam."*

Vilevile Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Daima kutakuwa na kundi miongoni mwa Taifa langu, watakaopigana kwenye upande haki, washindi juu ya kila wenye kuwakataa wao, hadi wa mwisho wao atakapopigana na al-Maseeh ad-Dajjaal."*

Twamalizia utafiti wetu kuhusu Mtume wa Allaah, 'Issa mwana wa Maryam, kwa kuitaja hadeeth ifuatayo. Abdullaah bin 'Amr bin al-'Aas amesema, Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"ad-Dajjaal atatokeza kwa Taifa langu na atakuwepo kwa (siku) arubaini* [Siku moja urefu wake ni kama Mwaka mzima, na siku ya pili itakuwa na urefu wa mwezi mzima, siku ya tatu itakuwa na urefu kama wiki nzima na zitakazobaki zitakuwa ni kama siku za kawaida]. *Kisha Allaah atamteremsha 'Issa mwana wa Maryam, atakuwa amefanana na 'Urwah bin Mas'ud, amtafute (ad-Dajjaal) apate kumuuwa. Kisha* [baada ya kufa kwa 'Issa atakaekuwepo kwenye ardhi kwa miaka arubaini, kama ilivyotajwa kwenye hadeeth iliyotangulia], *watu wataishi kwa miaka saba bila ya uadui baina ya watu wowote wawili. Allaah ataleta upepo mzuri wenye mzizimo kutoka ash-Shaam ambao hautomsaza* (hautombakisha) *mtu yoyote mwenye hata uzito wa chembe ndogo ya wema au Imani, isipokuwa hao* (wote watakufa). *Hata kama mmoja wenu atakuwa katikati ya mlima, utamfikia hapo alipo na umchukuwe* (roho yake). Kisha akasema: *"Watakaobaki hapo watakuwa ni watu waovu watupu. Watakuwa wepesi kama Ndege* [hawatokuwa ni waerevu]*, fahamu zao ni kama wanyama mwitu* [wakali na wakaidi]. *Hawatojua au hawatoamrisha wema wala kukataza au kujua uovu."*